



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU ASASI ZILIZOPEWA VIBALI VYA
KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA KATIKA UCHAGUZI MKUU WA
MWAKA 2020 KWA TANZANIA ZANZIBAR**

Zanzibar, 07 Julai, 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawafahamisha wananchi wote kuwa imekamilisha uchambuzi wa maombi ya asasi zilizoomba kupewa vibali vya kushiriki katika utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura kuhusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina jukumu la kutoa Elimu ya Mpiga Kura, kuratibu na kusimamia wadau wanaotaka kutoa Elimu ya Mpiga Kura Nchi nzima. Sheria hii pia inairuhusu kukasimu zoezi la utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura kwa Taasisi na Asasi zenye nia ya kutoa elimu hiyo. Kwa kuzingatia kifungu tajwa hapo juu, Tume huzialika Asasi zinazokusudia kutoa Elimu ya Mpiga Kura kuhusu michakato mbalimbali ya Uchaguzi, kuwasilisha maombi ya kupatiwa vibali vya kutoa elimu hiyo.

Hivyo, baada ya Tume kuzialika Asasi kuwasilisha maombi ya vibali kwa tangazo lililotolewa mwezi Novemba 2019, ilipokea maombi kutoka kwa Asasi mbalimbali za Kiraia zilizopo Tanzania Zanzibar. Katika uchambuzi wa maombi hayo, Tume ilibaini kasoro kadhaa kama vile baadhi ya asasi kukosa usajili kwa mujibu wa Sheria na taratibu.

Baada ya uchambuzi wa maombi hayo, Tume imeridhia kutoa vibali kwa Asasi 7 zilizokidhi vigezo vilivyowekwa kwa ajili ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura.

Tume inazitaka Asasi zote zilizopewa vibali kuzingatia taratibu na kanuni zinazoongoza zoezi hilo ikiwemo mwongozo wa utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura. Kwa muktadha huo, Asasi zote zilizopewa vibali kwa ajili ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura, zitalazimika kushiriki katika semina maalum ya kupitia mwongozo huo.

Vilevile, Tume inazitaka Asasi zilizopewa vibali kuwasilisha orodha kamili ya watendaji watakaoshiriki zoezi la utoaji Elimu ya Mpiga Kura, kuonesha maeneo halisi watakayotoa elimu hiyo na kuainisha vyanzo vya fedha.

Orodha kamili ya Asasi zilizopewa vibali itatangazwa kupitia vyombo vya habari na itapatikana pia kwenye tovuti ya Tume (www.nec.go.tz).

Imetolewa na:



Dkt. Wilson Mahera Charles

MKURUGENZI WA UCHAGUZI